Kwa Jina La Allaah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu

Al-Hudaa [Uongofu]

24th Sha'baan 1431
6th August, 2010

Volume 1, Issue 1

Al-hamdu lillah. Sifa zote njema na shukrani ni zenye kumthubutukia Allaah, Mola wa walimwengu. Tunamuhimidi na kumshukuru Yeye na kumtaka msaada na msamaha. Kwake Yeye tunajilinda na ushawishi wa nafsi zetu na makosa yetu. Yeyote ambae alieongozwa na Allaah (kwa Rehma Zake hawezi kupotolewa na yeyote. Na aliepotolewa na Allaah (kwa Hikma Zake) hawezi kuongozwa na yeyote. Nashuhudia yakwamba hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki illa Allah, peke yake, Asokuwa na mshirika na Muhammad (صلى الله عليه وسلم.) ni Mtume Wake.

Allaah (سبحانه وتعالى) ametubainishia ya kwamba kuandama kwa mwezi ndio njia ya pekee ya kuthibiti kwa tarehe na matukio ya kiislamu kama vile 'Idd na Hija. Na akasema:
Wanakuuliza juu ya miezi. Sema: "Hiyo ni vipimo vya nyakati kwa ajili (ya mambo) ya watu (mengine) na ya Hija (zao)." [Al-Baqarah (2):189]

Mtume (صلى الله عليه وسلم.) ametilia mkazo sana jambo la kuuona mwezi kongo, haswa katika kutambua mwanzo na mwisho wa mwezi wa Ramadhani. Imepokewa kutoka kwa idadi kubwa ya maswahaba (رضي الله عنه) kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم.) amesema:
"Fungeni (waislamu) mukiuona mwezi kongo. Ukifichikana, basi kamilisheni siku thalathini katika hisabu ya Sha'baan. Na mufungue muuonapo mwezi kongo. Ukifichikana, basi kamilisheni siku thalathini."[1]
Alikuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم.) akishughulika zaidi katika kuhakikisha kuandama kwa mwezi wa Sha'baan, kwa sababu ifikapo siku ya ishirini na tisa huutafuta mwezi wa Ramadhani au hukamilisha siku thalathini kabla ya kuanza kufunga. Ikapokewa kutoka kwa 'Aisha (رضي الله عنها):
"Alikuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم.) akishughulika sana kuhusu (kujuwa mwanzo wa) Sha'baan kuliko miezi mingine. Kisha alikuwa akifunga baada ya kuonekana (mwezi kongo wa) Ramadhani. Ukifichikana (mwezi) basi yeye huhesabu siku thalathini (za Sha'baan) kisha baadae akafunga."[2]

MASHAHIDI WANAOHITAJIKA:

MWEZI KONGO (CRESCENT)
HUTHIBITISHA TAREHE ZA KIISLAMU

Na sheikh Muhammad al-Jibaaly

Wanavyuoni wa kiislamu wamekubaliana ya kuwa mashahidi wawili wa kiislamu wanatosheleza ushahidi wao kuhusu kuandama kwa mwezi. Ushahidi wao umetokamana na riwaya kutoka kwa baadhi ya maswahaba (رضي الله عنهم yakwamba, amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم.):
"Waislamu wawili waadilifu wakiapa (kuwa wameuona mwezi) basi fungeni au fungueni saumu zenu."[3]
Wakakubaliana wanavyuoni wengi zaidi kuwa ushuhuda wa Muislamu mmoja utatosheleza kuhusu kuandama kwa mwezi. Dalili yao ni kwamba Ibn 'Umar (رضي الله عنهما) kuwa amesema:
"Watu walikuwa, wakiutafuta mwezi kongo (wa Ramadhani). Mimi nikampasha habari Mtume (صلى الله عليه وسلم.) yakuwa nimeuona mwezi. Kwa hivyo akafunga (siku iliyofuata) na akawaamrisha watu wafunge."[4]

USHAHIDI WA UTAALAMU WA NYOTA:

Hupatikana miongoni mwa watu ambao wanapendekeza kuhisabu masiku kulingana na ilimu ya nyota katika kuukadiria mwezi kongo. Hilo si jambo geni kwani lilizushwa jambo kama hilo katika nyakati za mwanzoni mwa Uislamu na Mtume (صلى الله عليه وسلم.) akalipinga. Ikapokewa kutoka kwa Ibn 'Umar رضي الله عنهما), yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم.) amesema:
"Sisi ni taifa lisilojuwa kusoma wala kuandika. Hatutumii maandishi wala hesabu za ilimu ya utaalamu wa nyota (katika kufunga). Mwezi ni kadha na kadha (akaashiria kwa mikono yake mara tatu, akakunja kidole cha gumba mara ya tatu, kumaanisha siku ishirini na tisa) au ni kadha na kadha na kadha (akaashiria kwa mikono yake mara tatu, kumaanisha siku thalathini)."[5]
Riwaya ya Abu-Dawud, ikaendelea zaidi:
"Kwa hivyo Ibn 'Umar alikuwa akimaliza kufunga na watu pamoja bila ya kuzitegemea hisabu za wataalamu wa nyota."
Hii inaonyesha vipi Mtume (صلى الله عليه وسلم.) alitaka kuifanya ibada hii iwe rahisi na pia iwe katika daraja ya watu wa kawaida. Ikaepushwa ibada kama hii na ilimu maalumu za ki-sayansi (iwapo ni za kweli au za shaka). Kwa sababu hii, ndipo akasema Ibn Taymiyyah (رحمه الله):
"Hali ya taifa hili ya kutojuwa kusoma na kuandika ni sifa, kwani lajitosheleza na kila matatizo katika utekelezaji wa misingi ya ibada."
Basi yoyote atakaepinga jambo hilo, huyo atakuwa amekwenda kinyume na 'ijmaa ya wanavyuoni wanaothaminika; atakuwa yuwajaribu kuchafua pambo na mipangilio ya dini hii, na hatari zaidi atakuwa ni mwenye kumuasi Mtume (صلى الله عليه وسلم.).

KUTOELEWEKA I: UHAKIKA WA MWANZO WA MWEZI

Jambo la kawaida lisiloeleweka na lenye umuhimu kwa watu wengi ni iwapo hatufanyi jitihada katika kukubali ushuhuda wa wale waliodai kuuona mwezi (kwa ushahidi wa wataalamu wa nyota na njia nyenginezo) basi huenda tukahatarisha kuzibatilisha baadhi ya ibada zetu kwa kufunga katika siku zisizostahiki. Mwenendo kama huu umekataliwa katika uislamu juu ya matukio mengi:

a. Jambo hili lahusiana na kutia shaka kuhusu ukweli (ushuhuda) wa Waislamu waadilifu (udul). Tumekatazwa kutokamana na (Nass ya) Qur'an na Sunnah.
b. Jambo hilo ni kwenda kinyume na Mtume (صلى الله عليه وسلم.) ambae aliekubali ushuhuda wa watu bila ya kukawiya na vile vile bila ya kuulinganisha ushuhuda huo na ushahidi wa utaalamu wa ilimu ya nyota.
c. Jambo hilo linafanana na tabia ya mayahudi ambao waliojikalifisha na sharia juu ya nafsi zao. Na Allaah akawaadhibu kwa kuzifanya

(Endelea katika Ukurasa wa 2)

Yaliyomo

Mwezi Kongo	1-2
Umuhimu wa Aqeedah	2-3
Matangazo	3
Ukumbi wa Kina mama Mama	4

Nukta Muhimu za Mazingatio:

1. Kutakuwa na Darsa za wanawake katika mwezi wa Ramadhaan, msikiti wa Mazrui, kuanzia saa Nne asubuhi mpaka Adhuhuri—kila siku isipokuwa ljumaa.
2. Jipatie Cd za Ustadh Na'maan kuhusu jinsi Älivyokuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) akifunga mwezi wa Ramadhaan. Na pia Cd za Mawaidha mbalimbali za ma-Duáat wetu.
3. Jipatie nakala ya vitabu vifuatavyo:

- Tafsiri ya Soorah Qaaf.
- Namna Ya Swala Ya Mtume (صلى الله عليه وسلم).
- Damu Asilia Za Wanawake.
- Na Risala nyenginezo zenye faida katika Dini.

Utayapata Yote hayo katika Maktaba ya QSS—Mombasa.

Umuhimu Wa Áqeedah

Sheikh Ábdul-Azeez al-Qaari

Mtume Muhammad صلى الله عليه وسلم alimwambia Mu'aadh bin Jabal alipokuwa katika safari ya kuelekea Yemen:
"Unakwenda kwa watu walio miongoni mwa watu wa Kitaab. Itakubidi ulinganizi wako wa kwanza kwao uwe ni wa kumuabudu Allaah. Iwapo watamkubali Allaah, basi wapashe khabari yakwamba Allaah Amewafaridhia juu yao, Swala tano katika nyakati zao za asubuhi na mchana." [al-Bukhari na Muslim]
Hadeeth hii iko wazi. Haihitaji wingi wa maelezo. Mtume صلى الله عليه وسلم aliitekeleza kanuni hii katika harakati zake za ulinganizi wa Da'wah katika Uislamu. Aliishi Makkah kwa muda wa miaka kumi na tatu, akiwafunza na kuwaelimisha maswahaba zake kuhusiana na Imaan na urekebishaji wa itikadi walizokuwa nazo. Hayo ndiyo malezi waliyo-lelewa nayo maswahaba.
Amesema Jundub ibn 'Abdullah al-bajaly, "Tumejifunza Imaan (kuamini), kisha tukajifunza Qur'aan ambayo (nayo) ikatuongezea Imani yetu." Nae 'Abdullah ibn 'Umar akasema: "Sisi tuliishi kwenye zama za wakati ambapo mmoja wetu aliipata Imaan mwanzo kabla hajaipata Qur'aan, na pindi Sura zilipokuwa zikiteremshwa tulikuwa tukijifunza maamrisho na makatazo yake na mambo yaliyohalalishwa na kuharamishwa na jinsi ya kukabiliana nayo. Lakini nimewaona watu wengi miongoni mwao walikuwa wanapewa Qur'aan kabla ya Imaan na akaisoma kuanzia mwanzo wake hadi mwisho wake asijue maamrisho wala makatazo yake - bila ya kuwa na mazingatio yoyote ya hiyo Qur'aan. Mfano wake ni kama mtu aliezitupilia mbali tende zake (usomaji wake wa Qur'aan haumfaidishi na chochote)."

Tumejifunza Imaan (kuamini), kisha tukajifunza Qur'aan ambayo (nayo) ikatuongezea Imani yetu.

Hii ndiyo desturi ambayo Mtume Muhammad صلى الله عليه وسلم aliyo-walelea nayo maswahaba zake: Imaan mwanzo na kisha Qur'aan. Hii inalingana na alivyoeleza Imaam Abu Hanifah (رحمه الله):
"Kuifahamu dini mwanzo (Tawheed) na kisha kuyafahamu ma'alumati yake (ya kisheria)."
Imaan ni sharuti zitakaswe mwanzo na baadae ifuate miradi mengine ya dini. Akasema nae Imaam ash-Shafi'i (رحمه الله):
"Mja yoyote atakaemuona Allaah na dhambi za aina yoyote, isipokuwa shirk, ni bora kuliko kuonana Nae (Allaah) hali ya kuwa juu ya Imani za uzushi."
Katika lugha ya kiarabu, neno 'Aqeedah limetokamana na neno 'aqadah. Kilugha (kiarabu) mtu anaweza kusema "'Aqada Kamba" ikiwa kamba imekazwa madhubuti. Na, "'Aqada bei" au Amekubaliana nae bei, ikiwa mtu ameafikiana na kuandikishiana mkataba kuhusu mapatano yao ya kibiashara. Na Allaah (سبحانه وتعالى) akasema katika Qur'an, (kama ilivyofasiriwa)

"Na wale mliofungamana nao ahadi wapeni sehemu yao ('Aqadat)" [Surat An-Nisaa (4):33].

Na pia Akasema tena Allaah, (kama ilivyofasiriwa)

"Lakini atakukamateni kwa viapo mlivyoapa na nia mlioifunga barabara ('Aaqadtum)" [Al-Maidah (5):89].

Aya hizi zinamaanisha uthibitisho na mafungamano na kitu fulani kama ilivyobainishwa kwenye aya isemayo, (kama ilivyofasiriwa)

"Na timizeni ahadi mnazozitoa kwa jina la Allaah mnapoahidi wala msivunje hizo ahadi baada ya kuzithubutisha hali mumekwisha mfanya Allaah kuwa Shahidi wenu. Hakika Allaah anayajua (yote) mnayoyafanya." [an-Nahl (16): 91

Mtu akisema, "Aqadtu kadhaa na kadhaa," maana yake moyo wake umethubutu juu ya kadhaa na kadhaa.
Kwahivyo 'Aqeedah au I'tiqaad kulingana na

(Endelea ukurasa wa 3)

Mwezi Kongo

(Endelea kutoka ukurasa 1)

hizo sheria ngumu zaidi. Akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم.):

"Jihadharini na (kuvuka mipaka) kuongeza mambo kwenye dini; kwa hakika waliokuwa kabla yenu waliangamizwa kwa kuongeza mambo katika dini."[6]

d. Jambo hilo laonyesha ujinga wa kutojua ni lini mwezi wa kiislamu huanza. Nukta hii, imeelezwa na Ibn Taymiyyah (رحمه الله):

"Watu wengi wanadhania ya kuwa mwezi mpya ukijitokeza mawinguni basi huo ndio usiku wa kwanza wa mwezi, bila ya kujali iwapo watu wameuona mwezi au la. Hayo ni makosa. Ni sharti mwezi huo ujitokeze kwa watu na watu wauone ili kuuanza mwezi. Ndio sababu ya Mtume (صلى الله عليه وسلم.) akasema: '(Uhakika wa) Saumu huanza ile siku muanzapo kufunga.'[7]
Ikamaanisha ya kwamba: hii ndio siku ambayo munayoitambua kama ndiwo wakati wa kufunga n.k. kwahivyo ikiwa nyinyi hamukuitambua siku hiyo basi hamutofaidika nayo."[8]
Rai hii imetiliwa mkazo na riwaya ifuatayo akasema Abu Al-Bakhturi, "Tulikwenda kufanya umra na tukaushuhudia (kuuona) mwezi kongo wa Ramadhani, tulipokuwa mahali paitwapo Dhatu 'Irq, ingawa mwezi wenyewe ulikuwa ni wa siku mbili au tatu. Kisha baadae tulipomuona Ibn 'Abbaas (رضي الله عنه) tukamueleza kuhusu jambo hilo nae Ibn Abbas (رضي الله عنه) akatuambia, "amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم.): Allaah amelifanya jambo la kuutazama mwezi kongo liwe ni alama ya Ramadhani. Kwa hivyo Ramadhani huanzia ule usiku muuonapo. Iwapo umefichamana nanyi basi kamilisheni hisabu."[9]
Jee, ikiwa wanaodai yakuwa wameuona mwezi walisema uwongo au walipitikiwa? Maadam uislamu wao ni wenye kudhihirika na ni waaminifu basi ni sharti kukubali ushuhuda wao na kuanza kufunga (au kufungua). Hatuna haki yoyote kukataa bila ya kuwa na ushahidi ulio wazi (unaoafikiana na sunnah kama ilivyoelezwa mbeleni). Iwapo walikuwa kweli wamekusudia kusema uwongo basi wao watastahiki madhambi peke yao, nasi tutakuwa (Insha-Allah) ni wenye kulipwa kheri zetu kwa kushikamana na sunnah.

(Endelea katika makala Yajayo)

... Damu Asilia

(Endelea kutoka ukurasa wa 4)

Swaum: (kufunga), Wakati wake inapostahiki na nyakati zake makhsusi katika mchana.

Hajj: Adabu za kula chakula, kunywa, kulala, mtu kujamiiyana na mkewe, kukaa, kuingia na kutoka nyumbani, jinsi ya kukidhi haja (kubwa na ndogo), hata idadi ya vijiwe vya kutumia katika *istijmar*, na mengi zaidi kwa utondoti kuhusuiana na chembe-chembe za aina ya vitendo mpaka matendo makubwa, ambayo kwayo Allaah (سبحانه وتعالى) ameikamilisha Dini Yake ya Uislamu na akakamilisha fadhla zake juu ya waumini kama Alivyosema (سبحانه وتعالى):

"Na tumekuteremshia wewe kitabu (Qur'an) chenye kuweka wazi kila kitu."

An-Nahl [16:89]

"Haikuwa Qur'an ni uzungumzi unaozuliwa lakini (Qur'an) ni yenye kusadikisha vitabu vilivyotangulia na ni upambanuzi wa kila kitu."

Yusuf [12:111]

(Endelea katika makala Yajayo)

Matangazo

Kwa Safari za Hajj, Al-Rahma Agencies, kutoka Mjini Mombasa, wanawatangazia Waislamu wote wenye niya ya kutekeleza Ámali hii Tukufu wajisajili katika afisi yao. Gharama za Safari ni $2,900.00 [US Dollars] - Kuanzia Mombasa mpaka Jeddah na Kurudi Mombasa; pamoja na Nyumba ya Kukaa [Makkah na Madinah] na Usafiri wa Ma-Bus. Na chakula [Mara Tatu kwa siku] katika siku za Mina kwa muda wa siku Tano. Msafara wetu Tutaandamana na Daktari [wetu] mpaka turudi nae Insha –Allaah. Darsa za maandalizi zitafanywa hapa [Mombasa] kabla ya kuondoka, na tukifika huko [Makkah].

Amma kwa upande wa kuchinja [udh-hiya] na chakula katika hoteli [Makkah na Madina] kila mtu ni juu yake. Kwa maelezo zaidi, wasiliana nasi kwa kutuandikia barua Pepe kwa info@qssea.net au kwa kutupigia simu namba zifuatazo.

+254 723471820, au +245 721473181 au +254 700365253

Umuhimu Wa Áqeedah

(Kutoka Ukurasa wa 2)

wanavyuoni wa ki-islamu ni: Imani thabiti iliyotulia juu ya moyo wa mtu pasi na kusita-sita au shaka yoyote. Haihusiki na dhana yoyote, shaka au tuhuma.
Imaam Abu Hanifa akaiita ilimu hii iliyo pana kwa jina la Fiqh-ul-Akbar ("Ufahamu Mkubwa") ambayo ndilo shina la kuifahamu dini hii. Na Kwahivyo 'Aqeedah au I'tiqaad kulingana na wanavyuoni wa ki-islamu ni: Imani thabiti iliyotulia juu ya moyo wa mtu pasi na kusita-sita au shaka yoyote. Haihusiki na dhana yoyote, shaka au tuhuma.
Imaam Abu Hanifa akaiita ilimu hii iliyo pana kwa jina la Fiqh-ul-Akbar ("Ufahamu Mkubwa") ambayo ndilo shina la kuifahamu dini hii. Na akayaita maarifa ya kisheria (Shar'ee), ujuzi wa kitaalamu. Wanavyuoni wengi wa kiislamu hutumia neno Tawheed kwa kila kinacho-fungamana na kuamini. Hii ni kwa sababu jambo muhimu zaidi hapa ni msingi wa Tawheed ulio kwenye matamshi ya, "Hapana apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah."
Kulingana na wao, Tawheed imegawanyika sehemu mbili: Tawheed ya kusadiki na kukiri na Tawheed ya makusudio na matendo. Tawheed ya kusadiki na kukiri ni Tawheed ya Upweke wa Mu-umba na Tawheed ya Majina Yake na Sifa Zake (hapana mshirika katika Uumba wake na ni Pekee katika majina Yake na Sifa Zake). Tawheed ya makusudio na matendo ni Tawheed ya Uola au kuwa hapana apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah (Yeye ndie wa Pekee anaestahiki kuabudiwa kwa haki).
Jee, katika Qur'aan, mas-ala haya yameitwa kwa jina gani?
Qur'aan imeyataja mas-ala haya makubwa kwa jina la "Imaan". akasema Allaah (سبحانه وتعالى) (kama ilivyofasiriwa):

"Na namana hivi tumekufunulia wewe (Muhammad) wahyi kwa amri yetu. Ulikuwa hujui Kitaab ni nini wala Imaan; Lakini tumefanya kitabu hiki (Qur'aan) ni nuru, ambayo kwa nuru hiyo Tunamuongoza Tumtakae..." [Ash-Shura **:52]**

Hapana shaka yoyote yakwamba nyoyo za waumini ni lazima ziwe thabiti juu ya "nguzo za Imaan". Na mtu yoyote hatoitwa mu'min kwa kujua na kufahamu nguzo hizo peke yake, lakini mpaka afikie daraja ambayo atakuwa anakiri (anakubali) na kutekeleza yanayompasa kama ilivyo-elezwa katika hadeeth ya Jibreel.
Kwahivyo Imaan katika hali hii imo ndani ya duara la Uislamu. Lau kama Imaan ni kuijua haki kwenye nyoyo tu, basi Shetani na Fir'auni pia wangelikuwa ni waumini [Alikuwa Shetani akimtambua Allaah kuwa n Mola wake, lakini aliangamizwa kwa ajili ya kiburi chake na wivu. Na Fir'auni nae, hata kama alidai Uungu, alikuwa anatambua yakwamba Mola ni Allaah na pia hapana anaestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah. Akatueleza Allaah (سبحانه وتعالى) katika Qur'aan (kama ilivyofasiriwa):

"Akasema (Musa): 'Bila shaka umekwishajua kuwa hakuna alieteremsha (hoja) hizi isipokuwa Mola wa Mbingu na Ardhi, kuwa dalili; (ila unajibabaisha tu)..."' [al-Israa':102]

Hata kama waliijua haki, lakini hawakuitekeleza kwa kuzielekeza 'ibada zao kwa Allaah peke Yake].
Katika hadeeth ya Jibreel, Mtume صلى الله عليه وسلم alizifafanua nguzo za Imaan hii ambazo inampasa kila kiumbe kuziamini. Alipoulizwa, "Ni nini Imaan?", akasema: "Ni kumuamini Allaah, na Malaika Wake, na Vitabu vyake, na Mitume Wake, na siku ya mwisho na kuamini Qadar (kheri yake na shari yake).

" Ni lazima juu ya kila mtu kuzijua nguzo hizi na kuzielewa kisawasawa na kuwa na Imani nazo kama walivyoamini na kuzielewa maswahaba wa Mtume صلى الله عليه وسلم na wafuasi wao. Vilevile wanahusika humo ma-Imamu wanne, Sufyaan ath-Thawree, Sufyaan ibn-'Uyaynah, 'Abdullah ibn al-Mubaarak na wengine kama hao na pia Muhammad ibn Ismaa'eel al-Bukhaari, Muslim ibn al-Hajjaaj, Sheikh ul-Islaam ibn Taymiyyah na al-Haafidh ibn al-Qayyim. Na wanavyuoni kama hao ambao waliofuata mwenendo huohuo wa kuziamini nguzo hizo.
Huu ndio wajibu wa kwanza alokabidhiwa mwana-adamu. Hapana ikhtilafu ya maoni juu ya suala hili miongoni mwa wanavyuoni ambao rai zao zinastahili kufuatwa. Akasema Imaam Abu Haneefah (رحمه الله):

"Kuifahamu (Ujuzi wa) Imaan ni bora kuliko kuyafahamu maarifa ya kisheria." Katika msemo huo aliikusudia Imani kuwa ni Tawheed na maarifa ya kisheria kuwa ni Hukmu za Kisheria. Akatanguliza kuifahamu Tawheed kabla ya kuzifahamu Hukmu za kisheria. Nae Sheikh al-Islaam al Haruwi al-Ansaaree (f.481 AH) akanukuu katika awali ya kitabu chake, *I'tiqaad ahl-as-Sunnah*:

"Wajibu wa kwanza unaompasa mja ni kumtambua Allaah. Jambo hili limethubutu kutokamana na Hadeeth ya Mu'aadh alipoambiwa na Mtume (صلى الله عليه وسلم):

"Unakwenda kwa watu walio miongoni mwa watu wa Kitaab. Itakubidi ulinganizi wako wa kwanza kwao uwe ni wa kumuabudu Allaah. Iwapo watamkubali Allaah, basi wapashe habari yakwamba Allaah Amewafaridhia juu yao, Swala tano katika nyakati zao za asubuhi na mchana...".

Kutoka katika chimbuko hili, wakatangulia wanavyuoni mashuhuri wa ki-Islamu. Hebu jaribu kuzingatia alivyofanya Imaam Muhammad ibn Ismaeel al-Bukhaaree katika kitabu chake "*al-Jaami' as-Saheeh*", ambacho ni kitabu bora zaidi kilicho saheeh baada ya Kitabu cha Allaah (al-Qur'aan). Utashangaa jinsi Allaah Alivyompa maarifa na Hikma nyingi katika kuifahamu dini. Imaam huyu mashuhuri, ameanzia kitabu chake na mlango wa "Mwanzo wa wahyi", kisha akafuatiliza na milango ya Imaan na baadae Ilimu. Ni kama alikuwa akituashiria, (رحمه الله); kwa kutujulisha yakuwa wajibu wa kwanza juu ya mwana-adamu ni Imaan (au kuamini), na haipatikani Imaan hiyo isipokuwa kwa ilimu. Na asili ya Imaan na ilimu ni wahyi (uteremsho). Akaanza kwa kutuonyesha vipi wahyi ulivyoteremshwa na baada ya hapo akazitaja Imaan na ilimu. Mipango hiyo haikuzuka tu kwa ajali bali pana mazingatio makubwa ndani yake. Haya ni jumla ya tulokusudia kuwadokezea na kwa ajili hiyo, tunazipaza sauti zetu. Mas-ala ya 'Aqeedah ni yenye kutangulizwa. Imani na ilimu ni njia za kuifikia. Na asili ya ilimu na Imani ni Kitaab (Qur'aan) na Sunnah.

P. O. Box 85477,
Mombasa,

E-mail: info@qssea.net

QSS (E.A)

جمعية القرآن والسنة في شريق إفرقيا

Tuko katika Tovuti
http://www.qssea.net

Ukumbi Wa Wanawake

Damu Asilia Za Kina Mama [Sheikh Muhammad bin Swaleh al-Uthaymeen] (رحمه الله)

Maana ya heidh

Katika lugha ya kiarabu, neno **Heidh** ni *kitu kumwagikacho au kuturuzika*. Kulingana na maana yake ya ki-Sheriya, ni damu inayomtoka mwanamke yenyewe bila ya sababu asilani ya nje, na (hutoka) katika nyakati maalumu. Kwahivyo, ni mturuziko wa damu usiohusiana na maradhi, jaraha, utoaji wa mimba wala mazazi. Tabia ya kutoka au kuturuzika kwake inadhihirika kutafautiana kwake miongoni mwa wanawake kulingana na hali zao kwa ujumla, mazingira na mahali alipo.

Hikma iliyoko inahusiana na ukweli yakwamba wakati wa kiinitete (embryo) kinapokuwa kwenye fuko (la mama) la uzazi huwa hakiwezi kupata virutubishi hata kutoka kwa mtu aliye na rehma za aina gani. Allaah (سبحانه وتعالى) ambaye ndiye Muumbaji Mkamilifu, aliumba mfumo wa damu yenye madini fulani inayopeleka virutubishi kwenye kiinitete kupitia katika kitovu. Hiyo ndiyo sababu mwanamke anapohimili mimba, damu yake ya mwezi husimama akawa hapati tena hiyo damu ya mwezi (Heidh)

Umri ambao heidh huanzia na kumalizikia

Kwanza: Jee, kuna muda maalum wa Umri?

Heidh hutokea baina ya umri wa miaka kumi na mbili na khamsini ingawaje mwanamke hwenda akaipata kabla au baada ya hapo kulingana na hali yake na mazingira. Ma-'Ulamaa (wanavyuoni) wa ki-Islamu, Rehma za Allaah ziwe juu yao wote, wamekhitilafiana iwapo kuna muda wa umri maalum ambapo heidh hudhihirika na kuhusu umbile la damu apatayo mwanamke kabla ya, au baada ya muda huu: Jee, damu yake hii ni ya heidh au ni damu isohusiana?

Baada ya kuzitaja rai tafauti kuhusu mas'ala haya, hatimae Imaam *ad-Daarimee* akamalizia: "kulingana na maoni yangu, wote wamekosea, kwa sababu maregeo ya yote hayo ni kuwepo au kukosekana kwa damu inayotoka bila ya kujali umri, na kwahivyo aina hii ya damu na ichukuliwe kuwa ni damu ya heidh, na Allaah Ndiye Mjuzi zaidi." Aloyasema ad-Daarimee ni msimamo wa sawa na pia hilo ni chaguo la *Sheikh Ul Islaam Ibn Taymiyyah*. Ilivyo ni kwamba, pindi mwanamke aonapo damu yake ya ada basi huwa ndio ashaingia kwenye Heidh hata kama umri wake hwenda ukawa ni chini ya miaka tisa au zaidi ya miaka khamsini. Hii ni kwa sababu Allaah (سبحانه وتعالى)na Mtume wake (صلى الله عليه وسلّم) wamefaradhisha hukmu ya heidh itumike itakapojitokeza heidh yenyewe na kulingana na hukmu hizi hapakutajwa mas'ala ya umri makhsusi wa kuanza au kumalizika kwa heidh. Kwa hiyo, *kubainisha muda wa umri fulani kunahitaji dalili kutoka katika Qur'an na Sunnah na hilo halipatikani.*

PILI: Muda wa Heidh

Kuna ikhtilafu kubwa miongoni mwa ma-'Ulamaa' kuhusu muda wa wakati ambamo mwanamke huzingatiwa kuwa katika heidh. Baadhi ya wanavyuoni wanasema: "Hakuna kuweka idadi ya masiku ya heidh ema nyepesi au nzito. Mtunzi huyu anasema: "Rai hii ni kama ile ya ad-Daarimee (iliyotangulia) na ndilo chaguo la Sheikh Ul Islaam Ibn Taymiyyah na ndiyo rai ya sawa kwa sababu, imethibitishwa na dalili kutoka katika Qur'an, Sunnah na ulinganifu mzuri:

Dalili No. 1:

Maneno yake Allaah (سبحانه وتعالى):

"Na wanakuuliza juu ya wanawake wenye (heidh), sema, huo ni uchafu. Basi jiepusheni na wake zenu wanapokuwa katika heidh na wala msiwakurubie (musiwaingilie) mpaka watwahirike (imalizike heidh)."

[al-Baqarah 2:222]

Ni wazi yakwamba Allaah aliifanya sababu ya kujiepusha kuingiliana kisheria (kujamiiyana) na mwanamke kuwa ni **ukosefu wa kutwahirika** katika wakati wa heidh yake na wala sio mwisho wa muda wa wakati maalum: Si mchana mmoja, wala si usiku mmoja, wala si siku tatu na wala si siku kumi na tano. Hii ni dalili yakwamba sababu ya hukmu ya Allaah ya hapo juu ni emma kupatikana kwa heidh (na madhara yake na uchafu) au kukosekana (hali ya kutwahirika).

Dalili No. 2:

Yaliyothibitishwa na Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلّم)katika kitabu saheeh cha hadeeth kiitwacho Saheeh al-Bukhaari, alipokuwa Mtume (صلى الله عليه وسلّم)akimueleza mkewe 'Aaisha (رضي الله عنهما) yanayompasa kufanya aingiapo katika ada yake akiwa amehirimia kufanya 'Umra:

"Fanya kila linalompasa mwenye kuhiji, isipokuwa tu usifanye Twawaaf (kulizunguka) al-Ka'bah mpaka utwahirike (kutokamana na heidh yako). Akasema: "Katika siku ya an-Nahr (siku ya kuchinja wanyama – tarehe 10 ya Dhul-Hijjah), nilitwahirika."

Vilevile imepokewa katika hadeeth nyengine (Saheeh al-Bukhaari) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلّم)alimwambia (yaani 'Aaisha):

"Subiri mpaka utwahirike, kisha uwende at-Tan'eem (Sehemu fulani iliyo Makkah) uhirimie (na baada ya kutekeleza 'Umra) kisha utakutana na sisi mahali kadhaa wa kadhaa ..."

Kwahivyo, Mtume (صلى الله عليه وسلّم) alibainisha waziwazi yakwamba sababu ya kumkataza 'Aaisha asitekeleze *ahkaam* za Hajj ni hali ya kutwahirika kwake na wala si muda maalum wa heidh yake. Hii inaashiria yakwamba hukmu ya ki-Islamu katika mas'ala haya inahusiana na kupatikana na kukosekana kwa heidh.

Dalili No. 3:

Makisio na maelezo kwa utondoti yanayotolewa na baadhi ya wanavyuoni kuhusu umri ambao heidh inapoanza na inapomalizika hayapatikani katika kitabu cha Allaah na katika Sunnah za Mtume (صلى الله عليه وسلّم) ingawa mas'ala haya ni ya dharura inayohitaji kubainishwa. Ikiwa ilikuwa ni wajibu kuyafahamu makisio hayo na kuyatumia katika kumuabudu Allaah, basi Allaah na Mtume wake wangeliyabainisha kwa kila mmoja. Hii ni kwa sababu ya umuhimu wa hukmu za ki-Islamu zinazo ongoza katika mas'ala mengi ya kumuabudu Allaah na ambayo hutegemea juu ya hali ya heidh, kwa mfano, Swala, Swaum, Ndoa, Talaka, Urathi na mengineo. Kama ijulikanavyo, Allaah (سبحانه وتعالى) na Mtume wake (صلى الله عليه وسلّم) wametueleza yafuatayo:

Swala: Idadi zake, nyakati zake, *Ruku'oo* zake, na Sujood zake.

Zakaat: Aina ya utajiri na mali zake,; *Nisaab*, viwango vyake, na wenye kustahiki.

(Endelea katika Ukurasa wa 2)